

Viwango vya Makosa ya Kisarufi katika Insha za Wanafunzi wa Mtaala wa Umilisi

Edmond Okiya^a, Frida Miruka^{a*}, Maurine Kangahi^b

^aIdara ya Elimu ya Lugha na Fasihi, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro, Kakamega, Kenya

^bIdara ya Elimu Chuo Kikuu cha Maseno, Maseno, Kenya

IKISIRI

KUHUSU MAKALA

Kiswahili ni miongoni mwa lugha za Kiafrika zilizothaminiwa na kupewa nafasi muhimu katika mtaala wa umilisi nchini Kenya. Vilevile ni lugha yenye dhima kuu ya kutagusanisha watu katika jamii. Lugha hii hata hivyo hukumbwa na changamoto anuwai. Mojawapo ya changamoto hizi ni athari ya lugha ya kwanza kwa ujifunzaji wake. Hali hii huathiri wanafunzi katika viwango vyote vya elimu ikiwemo shule za msingi na hudhihirika kwa jinsi mbalimali ikiwemo ukiukaji wa sheria za kisarufi katika uandishi wa insha za wanafunzi. Lengo la makala hii ni kuchunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi katika mtaala mpya wa elimu ya umilisi. Makala hii inajikita katika nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa ya [Corder \(1974\)](#) na [Sridhar \(1981\)](#). Data ilikusanywa maktabani kwa kudurusu insha za wanafunzi na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo yanaonyesha kuwa makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi katika mtalaa wa umilisi hubainika katika viwango vyote vya sarufi sauti, sarufi maumbo, sarufi miundo na sarufi maana. Chanzo kikuu cha makosa haya ni athari ya lugha ya kwanza. Makala inapendekeza kuwa uimarishaji wa mikakati ya kufunza insha na uhamasishaji wa wazazi ni miongoni mwa njia za kupunguza makosa haya.

Maneno Makuu:

Insha,
Makosa ya kisarufi,
Mtaala wa Umilisi.

Historia ya Makala:

Tarehe ya Kutumwa: 10 Januari 2025
Tarehe ya Kurekebisha: 25 Aprili 2025
Tarehe ya Kukubalika: 10 Juni 2025
Mtandaoni: 29 Agosti 2025

1. Utangulizi

Lugha za binadamu huwa na mpangilio maalumu wa sauti zilizokubaliwa na wanajamii fulani ili zitumike katika mawasiliano yao ([Kiango, 2002](#)). Dhana ya lugha kwa jumla inajidhihirisha bayana katika mhimili wa mawasiliano; kwa maana kuwa, lugha ni chombo cha mawasiliano kati ya binadamu na binadamu au jamii na jamii katika eneo fulani kama kabila au taifa. Hivyo basi, jukumu la kutimiza dhima ya kukidhi haja ya mawasiliano katika jamii kupitia lugha haliwezi utatimia kama chombo hicho (lugha) hakiijaundiwa utaratibu maalumu. Utaratibu huo huundwa na wanajamii kwa lengo la kuweka kaida au sheria zinazopaswa kuwaongoza watumiaji wa lugha hiyo ili kuweza kufikisha ujumbe unaoeleweka. Utaratibu huo ndio unaoitwa sarufi ya lugha fulani. ([Mushumbwa, 2020](#)). Kanuni hizo huwaongoza watumiaji wa lugha hiyo katika kutumia lugha kwa usahihi ikiwa ni pamoja na kuunda tungo sahihi na zinazokubalika katika mfumo wa lugha ya jamii fulani. Licha ya kuwepo taratibu hizi, hali na miktadha mbalimbali husababisha ukiukaji wa kaida hizo na kutokea makosa ya kisarufi. Lengo la makala hii ni kuchanganua viwango vya makosa ya kisarufi katika insha

za wanafunzi wa mtaala wa umilisi katika kaunti ndogo ya Butula.

Sarufi ni taaluma ya uchambuzi wa lugha katika viwango vyote vya uchambuzi yaani umbo sauti (fonolojia), umbo neno(mofolojia), miundo maneno(sintaksia) na umbo maana (semantiki) ([Massamba na wenzake, 2009](#); [Bakita, 2015](#)). Massamba na Wenzake wanaongeza kuwa Sarufi ni sheria zinazotawala hivi viwango vinne vya uchambuzi wa lugha. Hivyo, dhana ya sarufi hugawika katika viwango vinne mtawalia mathalani sarufi sauti, sarufi maumbo, sarufi miundo na sarufi maana. Makala hii imeangazia makosa ya kisarufi katika viwango vyote vya sarufi katika mtaala wa umilisi.

Kulingana na ratiba ya mtaala mpya wa elimu ya umilisi nchini Kenya, mfumo wa umilisi wa 6-3-3-4 ulianza kutekelezwa kuanzia mwaka wa 2017 ukichukua nafasi ya mfumo wa 8-4-4. Lugha za asili zimeungwa mkono kimatumizi katika mtaala wa elimu ya umilisi ili kuimarisha ufunzaji. Katika mtaala wa elimu ya umilisi wazazi walishirikishwa katika mafunzo ya wanao ilihali

* Mwandishi Mkuu. Simu: +254100134928; Barua Pepe: edmondokiya@gmail.com

Mhariri: Pamela Ngugi, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.

Nukuu: Edmond O., Frida M., & Maurine K. (2025). Viwango vya Makosa ya Kisarufi katika Insha za Wanafunzi wa Mtaala wa Umilisi. Jarida la Kiswahili Sanifu, 2(1), 21 – 29.

hawakuhamasishwa na serikali kuhusu ufunzaji huu. Hali hizi zimechangia athari ya lugha asilia ya kimarachi kwa ufunzaji wa Kiswahili. Eneo la utafiti huu, Kaunti ndogo ya Butula, inapatikana katika kaunti ya Busia nchini Kenya. Ni eneo lenye wasemaji wa lugha ya Kimarachi mojawapo ya lahaja za kiluhya ambayo ni miongoni mwa lugha za kibantu. Lugha asilia ya wanafunzi wengi katika eneo hili ni Kimarachi. Kwa hivyo kimarachi kama lugha asili inakubalika kimatumizi na kiufunzaji kutokana na mtaala wa elimu ya umilisi. Kulingana na utafiti wa awali, muingiliano na muathiriano wa Kimarachi na Kiswahili ulikuwa mojawapo ya sababu za makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa shule za msingi. Ni katika msingi huu ambapo Makala hii inaangazia makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa mtaala wa umilisi katika kaunti ndogo ya Butula.

1.1. Suala la Utafiti

Lugha ya Kiswahili ina asili yake katika lugha za kibantu (Guthrie 1971). Kwa hivyo inahusiana na lugha nyingine za Kibantu katika vipengele mbalimbali ikiwemo sarufi. Kimarachi ni mfano wa lugha hizi inayozungumzwa katika kaunti ndogo ya Butula. Kwa vile Kiswahili ni lugha ya kibantu pamoja na hali kwamba lugha asilia imepewa kipaumbele katika mtaala wa umilisi, inatarajiwa kuwa wakaazi wa eneo hili wawe na ujuzi mwafaka wa Kiswahili na kuitumia ipasavyo. Kwa hivyo wanafunzi wa gredi ya sita wa shule za msingi kaunti ndogo ya Butula wanatarajiwa kuwa na ujuzi wa lugha ya Kiswahili. Hata hivyo kinyume cha hali hii kimeshuhudiwa. Hali hii imeathiri ufunzaji wa lugha ya pili (Kiswahili) hali ambayo inawafanya wanafunzi katika eneo hili kufanya makosa katika mazungumzo na maandishi ya insha. Mtaala mpya wa elimu ya umilisi umeipa nafasi ufunzaji wa matumizi ya lugha ya kwanza ikiwemo Kimarachi. Hali inayotarajiwa kuimarisha lugha ya Kiswahili. Wazazi walikuwa na mchango wa kuwasaidia watoto katika masomo yao ya shuleni ingawa serikali haikuwahamasisha kuhusu nafasi yao katika mtaala wa elimu ya umilisi. Katika misingi hii, makala hii ililenga kuchunguza viwango vya makosa ya kisarufi katika uandishi wa insha za Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi katika mtaala wa elimu ya umilisi.

2. Uhakiki wa Maandishi

Wataalam mbalimbali wameangazia suala la makosa ya kisarufi katika tanzu mbalimbali za sarufi. Kazi nyingi hata hivyo zimeangazia makosa ya kifonolojia. Nyagah, (2016) anaeleza makosa ya udondoshaji wa sauti, uchopekaji sauti na utumiaji mbadala wa sauti. Vipashio hudondoshwa katika silabi, neno, kirai au kishazi na kusababisha makosa kwa wajifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Anatoa mifano kama udondoshaji wa sauti /h/, kama vile; *akuna badala ya hakuna, udondoshaji wa nazali /n/; *dugu badala ya ndugu na udondoshaji wa nazali /m/; *matebezi badala ya matembezi. Vilevile, anaonyesha namna sauti za irabu, konsonanti na kiyeyusho huchopekwa katika neno katika mazingira ambapo sauti hizo hazistahili na kusababisha kutokea kwa makosa. Mchakato huu huchangia makosa kama matumizi ya sauti /s/ badala ya /z/ kama vile *kupotesa

badala ya kupoteza na *ulisa badala ya uliza. Pia kunaweza kutokea kuchanganya sauti.

Kwa mujibu wa Akoth (2014), kila lugha huwa na mfumo fulani wa sauti mahususi ambao unastahili kufuatwa ili kufanikisha mawasiliano. Kutozingatiwa kwa mfumo huo ndio husababisha makosa mengi katika tungo za wanafunzi. Makosa ya kisarufi huathiri matamshi au sauti za lugha mahususi (Mashaka, 2015). Kutokana na utafiti wake wa fonolojia ya lugha ya Kijita na Kiswahili, Mashaka aligundua kuwa lugha hizi mbili zinaingiliana pakubwa sana. Kuingiliana huku husababisha ukiukaji wa kanuni za kisarufi za lugha ya Kiswahili ambapo sauti hutamkwa au kuandikwa visivyo. Anataja udondoshaji wa sauti na matumizi ya sauti mbadala kama mifano. Wanafunzi wa Kijita hudondosha sauti /h/ katika baadhi ya maneno na kuandika miundo isiyofa kama vile *ajaenda badala ya hajaenda.

Otiende (2013) anabainisha makosa ya uchopekaji na matumizi mbadala ya sauti. Kutokana na utafiti wake kuhusu fonolojia ya Kiswahili na Olusuba, aligundua kuwa kuna tofauti kati ya miundo ya maneno fulani. Tofauti hizo huathiri matumizi ya Kiswahili kwa kiwango fulani kimatamshi na kimaandishi ambayo husababisha wanafunzi kufanya makosa kama vile; makosa ya uchopekaji wa irabu /u/ mfano *mutu badala ya mtu, *mugeni badala ya mgeni. Kwa hivyo mzungumzaji wa Olusuba kama L1 anapoitumia Kiswahili anaishia kudhihirisha athari za sauti nyingine katika kuitamka na kuandika sauti hii kimakosa. Wairimu (2016) anasema kuwa wanafunzi wa Kiamu wanapoandika baadhi ya maneno huacha sauti fulani nje hali ambayo husababisha makosa ya kifonolojia katika Kiswahili. Mara nyingi wanafunzi wa Kiamu wanaojifunza Kiswahili hudondosha konsonanti /l/ katika baadhi ya maneno inapotokea katikati ya irabu mbili na kusababisha makosa.

1.2. Misingi ya Nadharia





Makala hii inaongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ili kubainisha viwango vya makosa yanayojitokeza katika insha za wanafunzi wanaojifunza Kiswahili katika mtaala wa elimu ya umilisi wa shule za msingi katika kaunti ndogo ya Butula. Kisakwah (2014) akimnukuu Corder (1967) anasema Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ina mihimili ambayo inastahili kufuatwa katika uchanganuzi wa makosa. Hatua zifuatazo ni muhimu: Kukusanya sampuli ya kazi ya wanaojifunza lugha, kutambua makosa, kuainishana kufafanua makosa, kutathmini na kufafanua vyanzo vya makosa ya kisarufi na utathmini makosa na kusahihisha makosa haya ili kujua jinsi ya kukabiliana nayo. (Coder, 1974; Al-Khreshel, 2016). Katika Makala hii, Sampuli ya kazi ya insha ilikusanywa, makosa ya kisarufi yakatambuliwa na kuainishwa katika kategoria za kisarufi za sarufi sauti, sarufi maumbo, sarufi muundo na sarufi maana.

3. Mbinu za Utafiti

Utafiti ulitumia mkabala wa kithamano kueleza suala la uchanganuzi makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi. Marshall (1996), anashadidia umuhimu wa mkabala huu katika uchunguzi wa kina. Kutokana na

mkabala huu utafiti ulihusisha muundo wa usoroveya elezi kuchanganua aina za makosa ya kisarufi yaliyodhihirika katika insha. Muundo huu ulikuwa muhimu katika kupata data ya mazoea, masuala ya elimu

na kijamii (Kombo & Tromp, 2006). Kundi lengwa lilikuwa walimu na wanafunzi wa Kiswahili wa gredi ya sita. Usampulishaji wa kimaksudi ulitumika kuchagua shule za



Tak. 1: Makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi

kutwa za msingi, wanafunzi na walimu wa kiswahili walioshirikishwa katika utafiti huu kutoka kila shule. Usampulishaji wa kitabakishi ulitumika kugawa shule katika makundi kama vile shule za wasichana za kutwa, shule za wavulana za kutwa na shule za mseto za kutwa. Usampulishaji nasibu ulitumika katika kuchagua wanafunzi waliohusishwa. Mbinu ya uchanganuzi wa nyaraka ilitumika kukusanya data katika insha za wanafunzi katika shule za msingi za kutwa zinazotumia mtaala wa elimu ya umilisi. Kupitia kwa mbinu hii mtafiti alibaini viwango mbalimbali vya makosa ya kisarufi

viliyojitokeza katika insha za wanafunzi wa shule za msingi. Data ya utafiti ilipangwa katika dhamira na kuwasilishwa katika maJed. na maelezo katika aya mbalimbali.

4. Matokeo na Mjadala

4.1. Makosa ya Kisarufi katika insha za Wanafunzi

Uchunguzi wa insha za wanafunzi wa mtaala wa elimu ya umilisi, kaunti ndogo ya Butula, gredi ya sita ulibaini makosa mabimbali: udondoshaji wa sauti,

uchopekaji wa sauti, ubadilishaji wa sauti, utenganishaji wa neno, uunganishaji wa neno, makosa ya upatanisho wa sarufi, matumizi ya msamiati usiofaa na mrundiko wa maneno katika sentensi. Makosa yaliyojandikwa yanatokana na data ifuatayo miongoni mwa nyingine. Utafiti ulizingatia mihili ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa katika uchanganuzi wa data kama wanavyoeleza Corder (1967) na Al-Khreshel (2016). Uchanganuzi huu ulianza kwa ukusanyaji wa sampuli ya kazi za wanafunzi zifuatazo:

Makosa katika kazi hizi yalitambuliwa na kupigiwa mistari kama wanavyopendekeza Corder (1967) na Sridhar (1981). Baada ya kupigiwa mistari makosa yaliainishwa na kuchanganuliwa kulinganana na mihimili ya NUM.

4.2. Makosa ya sarufi sauti

4.2.1. Udondoshaji wa sauti

Massamba (2016:131) anaeleza kwamba udondoshaji ni utaratibu wa kutoa kipashio fulani cha kiisimu katika silabi, neno, kirai na kishazi.

Udondoshaji wa Konsonanti /w/

Kutokana na matokeo ya utafiti, kosa la kwanza la sarufi sauti katika insha za wanafunzi lilikuwa udondoshaji wa sauti /w/. Jed. 1 linaonesha maneno yenye athari ya udondoshaji yaliyotokana na insha za wanafunzi.

Jed. 1: Udondoshaji wa Konsonanti /w/

Neno sahihi	Neno lenye athari
Alikuwa	Aliku ^a
Huwa	Hu ^a
Mweupe	M ^a eupe
Mwembe	M ^a embe
Mwimbaji	M ^a imbaji

Jed. 1 linaonyesha udondoshaji wa sauti /w/. Sauti hii ilidondoshwa pale ambapo ilifuatana na sauti mwambatano na pale ilitokea katikati ya irabu. Kutokana na data yetu makosa mengi ya udondoshaji wa sauti /w/ yalitokea wakati sauti hiyo inatoka katikati ya irabu mbili kama vile: (alikuwa* badala ya alikuwa, hua* badala ya huwa) Ukosefu wa umilisi bora wa lugha ya Kiswahili uliwapelekea wanafunzi kufanya makosa ya udondoshaji wa sauti /w/.

Udondoshaji wa sauti /a/

Insha za wanafunzi pia zilionesha udondoshaji wa sauti /a/ wakati ilitokea katikati ya konsonanti mbili na mwishoni mwa neno panapo mfuatano wa irabu mbili; mifano katika Jed. 2.

Jed. 2: Udondoshaji wa Irabu /a/

Neno sahihi	Neno lenye athari
Wakati	wak ^a ti
Nilimpata	nilimp ^a ta
Inavutia	Inavuti ^a
Masomo	M ^a somo
Waliandaa	waliand ^a

Udondoshaji wa irabu /a/ ulipofanywa na mwanafunzi ulibadilisha maana ambayo mwanafunzi alilenga kuwasilisha. Katika Jed. 2, mwanafunzi alilenga kusema, “Anapenda masomo” akaishia kusema,

“Anapenda msomo”. Katika utafiti huu lugha ya Kiswahili na ya Kimarachi zote zinatumiwa silabi wazi kwa hivyo hali hii haitarajiwi. Kutokea kwa hali hii ni ishara ya kutomudu matumizi ya Kiswahili ipasavyo.

Udondoshaji wa Konsonanti /h/

Kutokana na data ya utafiti huu, konsonanti /h/ ilidondoshwa katika mazingira ya kufuatiwa na irabu. Jed. 3 linaonesha mifano ya maneno yenye athari ya udondoshaji wa konsonanti /h/ kama yalivyotokea katika insha za wanafunzi.

Jed. 3: Udondoshaji wa Konsonanti /h/

Neno sahihi	Neno lenye athari.
Hisabati	isabati
hapendi	Apendi
Huheshimu	ueshimu
uhusiano	uusiano
Hakuna	akuna
Huzuni	uzuni
Asubuhi	asubui

Mifano katika Jed. 3 inaonyesha udondoshaji wa /h/. Utafiti huu ulibaini kuwa katika lugha ya Kimarachi, hakuna sauti /h/ hali ambayo ingeathiri matumizi yake katika lugha ya Kiswahili kwa kuidondosha au kupachika pasipostahili katika mazungumzo au maandishi. Hali hii ilikuwa dhahiri katika insha.

Udondoshaji wa Irabu /i/

Kosa la nne la sarufi sauti katika maandishi wa insha za wanafunzi lilikuwa udondoshaji wa irabu /i/. Mifano imetolewa katika Jed. 4:

Jed. 4: Udondoshaji wa Irabu /i/

Neno sahihi	Neno lenye athari.
Wasichana	was ^a chana
nilimpita	Nilimp ^a ta
Kutimia	kut ^a mia
Kukimbia	kuk ^a mbia
Kufanikiwa	kufan ^a kiwa
Shinikiza	shin ^a kiza

Makosa katika Jed. 4 yalidhihirika wakati irabu /i/ ilitokea katikati ya sauti mbili za konsonanti kama inavyodhihirika katika Jed. 4. Katika neno nilimp^ata konsonanti mbili zinazorejelewa ni /p/ na /t/. Kutokana na utafiti wanafunzi wazungumzaji wa Kimarachi walishindwa kujua ni wakati upi watumie sauti /i/ na ni wakati upi wasiitumie jambo ambalo liliwapelekea kufanya makosa. Kama wanavyoeleza Sridhar (1981) kuhusu daraja za uchanganuzi makosa, utafiti uliainisha udondoshaji kama mojawapo ya makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi.

Jed. 5: Uchopekeji wa Irabu /u/

Neno sahihi	Neno lenye athari.
Mtu	Mutu
Mvulana	muulana
mchwa	Muchwa
Mnapenda	munapenda

4.2.2. Uchopekaji wa sauti.

Kosa la pili la sarufi sauti lilikuwa uchopekaji. Nyagah (2016) anaeleza uchopekaji kama uingizaji wa irabu, kiyeyusho au konsonanti katika neno fulani na kupelekea makosa katika neno hilo. Makosa ya uchopekaji yalidhihirika katika insha za wanafunzi

ambapo wanafunzi walifanya makosa ya kuchepeka sauti mwanzoni, katikati na mwishoni mwa maneno ya lugha ya Kiswahili. Uchopekeji wa sauti zifuatazo ulitokea:

Uchopekaji wa Irabu /u/

Irabu /u/ iliongezwa katikati ya neno hasa maneno yenye sauti mwambatano kama vile neno [mutu] badala ya [mtu]. Mifano zaidi ipo katika Jed. 5. Uchopekaji huu ulivuruga usanifu wa maneno ya lugha ya Kiswahili. Jed. 5 linaonyesha irabu /u/ ilichopekwa katikati ya konsonanti mbili wakati konsonanti tangulizi ikiwa kama silabi funge. Katika neno [mchwa] kwa mfano, wanafunzi walifanya makosa ya kuongeza herufi /u/ kwenye silabi funge /m/ na kuwa [muchwa]. Kutokana na utafiti huu hali hii ilitokana na sababu kuwa silabi nyingi za Kimarachi kama za Kiswahili ni wazi, kwa hivyo wanafunzi hawatambui silabi funge na hawajui wakati upi irabu iongezwe kwenye konsonanti na ni wakati upi isiongezwe.

Uchopekaji wa Irabu /i/

Uchopekaji wa irabu /i/ pia ulitokea. Irabu hii ilichopekwa katika maneno yenye asili ya kigeni kama vile katika neno [dakitari]. Mifano imeonyeshwa katika Jed. 6.

Jed. 6: Uchopekeji wa Irabu /i/

Neno sahihi	Neno lenye athari.
Alishtuka	alishituka
daktari	Dakitari
Askari	asikari

Kutokana na utafiti huu hakuna muundo wa silabi funge katika lugha ya Kimarachi hali hii inachangia wanafunzi wazungumzaji wa Kimarachi kuchepeka sauti /i/ katika baadhi ya maneno na kusababisha makosa

4.2.3. Utumiaji wa Sauti Mbadala

Watafitiwa walibadili sauti na nyingine mahali pasipofaa. Ubadilishaji huu wa sauti ulifanya neno husika kupoteza maana iliyokusudiwa kuwasilishwa. Nyagah (2016) anaeleza kuwa utumiaji mbadala wa sauti, ni mbinu ambapo sauti ambayo haipatikani katika mfumo wa lugha fulani inabadilishwa na sauti nyingine au sauti inayokaribiana nayo. Mchakato huu ulichangia makosa katika insha za wanafunzi kama ifuatavyo:

Matumizi ya Irabu /i/ badala ya /a/

Ubadilishaji huu umejitokeza mwishoni na katikati mwa neno hasa inapotokea baada ya konsonanti. Jed. 7 lifuatalo linaonyesha kuwa wanafunzi walitumia irabu /i/ mahali sauti /a/ ilistahili kutumiwa:

Jed. 7: Matumizi ya Irabu /i/ badala ya /a/

Neno sahihi	Neno lenye athari.
Kiranga	kiranji
Upande	Upinde
Anapenda	anapendi
Ujasiri	Ujisiri
Unaielekeza	unielekeza

Wanafunzi walifanya makosa ya ubadilishanaji wa /a/ kuwa /i/. Ubadilishaji huu huweza kupotosha maana iliyokusudiwa katika neno, kama vile neno [upinde] lina maana tofauti na neno [upande] Obara (2014) katika uchanganyuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi

wazungumzaji wa lugha ya ekegusii, anasema kuwa maingiliano baina ya lugha ya Ekegusi na Kiswahili husababisha ukiukaji wa kanuni za kisarufi za lugha ya Kiswahili ambapo sauti hutamkwa au kuandikwa visivyo. Pia wanafunzi huweza kuhamisha sauti aliyoizoea katika lugha yake ya kwanza kwenda lugha ya Kiswahili. Wakati mwingine wao huchanganya matumizi ya sauti kwa sababu ya kuathirika na lugha ya Kwanza.

Matumizi ya Irabu /i/ badala ya /u/

Wanafunzi walifanya makosa ya kutumia Irabu /i/ badala ya irabu /u/ katika uandishi wa insha. Jed. 8 linaonyesha mageuzi ya irabu /u/ kuwa /i/ mwanzoni mwa neno kama vile [ugonjwa ikaisha] na katikati mwa neno kama vile [anaipenda].

Jed. 8: Matumizi ya Irabu /i/ badala ya /u/

Neno sahihi	Neno lenye athari.
Anaupenda	Anaipenda
Vile ulivyo	Vile ilivyo
Mwiko ukavunjika	Mwiko ikavunjika
Ugonjwa ukaisha	Ugonjwa ikaisha
Uliimbwa	iliimbwa

Jed. 8 linaonyesha ubadilishaji wa sauti /i/ na sauti /u/ kutokana na hali kuwa walishindwa kutambua miundo na matumizi ya ngeli ya U-I jambo ambalo lilisababisha makosa katika insha zao.

Matumizi ya Konsonanti /y/ badala ya /l/

Kutokana na data yetu sauti /y/ imetumika kwa mazingira ya sauti /l/ inapofwatiwa na irabu. Mchakato huu ulidhihirisha makosa haya kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo katika Jed. 9.

Jed. 9: Matumizi ya konsonanti /y/ badala ya /l/

Neno sahihi	Neno lenye athari.
Jina lao	Jina yao
Jina la	Jina ya
Somo la	Somo ya
Penzi lake	Penzi yake
Kanisa la	Kanisa ya

Katika Lugha ya Kimarachi sauti /l/ haipo ilhali kunayo sauti /y/ hali ambayo inafanya wanafunzi wachanganyikiwe wasijue wapi watumie sauti /l/ na wapi wasiitumie. Sababu hii huwapelekea wanafunzi kufanya makosa. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Wenceslaus (2015) aliyegundua kuwa wanafunzi hutatizika sana kwa sababu sauti walizozizoea katika lugha ya Kijita hazipatikani katika lugha ya Kiswahili au zile zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili hazipatikani katika lugha ya Kijita.

Matumizi ya sauti /y/ badala ya /w/

Kutokana na utafiti, chanzo cha makosa haya ni kwamba wanafunzi wengi wasemaji wa Kimarachi hawana umilisi toshelevu wa ngeli za Kiswahili, hali ambayo husababisha makosa ya udadilishaji wa /y/ na /w/ kama katika Jed. 10:

Jed. 10: Matumizi ya /y/ badala ya /w/

Neno sahihi	Neno lenye athari.
Mwili wake	Mwili yake
Mpira wa	Mpira ya
Ukarimu wake	Ukarimu yake
Wimbo wote	Wimbo yote

Sauti hizi zilibadilishwa katika vivumishi vimilikishi vya -a unganifu mwanzoni mwa neno kama inavyodhihirika katika Jed. 10. Kosa hili hutokana na ukosefu wa umilisi wa ngeli ya U-I, U-U na U-ZI. Kutokana na Jed. 9, Ukosefu wa umilisi wa ngeli ya U-I uliwapotelekea wanafunzi kufanya makosa na kuandika [mwili yake] badala ya [mwili wake], [mpira ya] badala ya [mpira wa]. Makosa katika ngeli ya U-U ni [ukarimu yake] badala ya [ukarimu wake] kisha makosa katika ngeli ya U-ZI ni kama vile [wimbo yote] badala ya [wimbo wote].

Matumizi ya Konsonanti /th/ badala ya /dh/

Jed. 11 lifuatalo linaonyesha namna ubadilishai wa /th/ na /dh/ ilitokea katika insha za wanafunzi:

Jed. 11: Matumizi ya Konsonanti /th/ badala ya /dh/

Neno sahihi	Neno lenye athari.
Dhababu	Thhababu
Vidhibiti	Vithibiti
Madhehebu	Mathehebu
Nilidhalilishwa	Nilithalilishwa
Kumdhalimu	Kumthalimu

Kutokana na data katika Jed. 11 wasemaji wa lugha ya Kimarachi wanaojifunza lugha ya Kiswahili, walitumia konsonanti /th/ katika mazingira ya /dh/ inapowatiwa na irabu. Hali hii husababisha makosa ambayo huvuruga maana na ujumbe uliokusudiwa kupitishwa. Wanafunzi hawakuelewa ni wapi watumie konsonanti /th/ na ni wapi watumie /dh/. Kulingana na utafiti, kutoelewa matumizi ya konsonanti hizi mbili kuliwasababishia makosa katika insha zao. Ubadilishaji wa sauti huweza kuzalisha neno tofauti na kusababisha upotofu wa maana ya neno kama vile neno [vidhibiti] kuwa [vithibiti]. Maneno haya yana maana tofauti, mwanafunzi alidhamiria kutumia neno vidhibiti akaishia kuandika neno hilo kuwa vithibiti na kubadilisha maana aliyokusudia.

Utafiti huu ulibaini kuwa baadhi ya sauti za Kiswahili hupitia mageuzi na kudhihirisha makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa Kimarachi wanapojifunza kiswahili. Corder (1967) anaeleza kwamba makosa mengi ya wajifunzaji wa lugha ya pili yanatokana na wajifunzaji wenyewe kutumia kimakosa kanuni za lugha ya pili wanayojifunza. Kwa mujibu wa Cross (2009) wanafunzi wa Kijapani wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya pili waliathiriwa na lugha yao ya kwanza wakawa na shida katika kutofautisha sauti /b/ na /v/, waliziunganisha sauti hizi mbili na kuzitamka kama /v/ ya Kijapani. Aidha utafiti wake ulionesha kuwa kuna haja ya kushughulikia athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ilitumika kutambua makosa ya kisarufi na kuyaweka katika kategoria ya fonolojia jinsi anavyoelekeza Corder (1967).

4.3. Makosa ya Sarufi Maumbo

Omar (2022) akinukuu Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (KSIL, 1990:40) anaeleza kuwa sarufi maumbo ni kiwango au kipengele cha sarufi ambacho hujikita katika uchunguzi wa maumbo ya maneno kwa kuzingatia uchunguzi wa miundo (jinsi maneno yanavyoundwa) ya

maneno, makundi ya maneno na uhusiano wa maneno pamoja na taratibu za uundaji wa maneno. Wanafunzi wa mtaala wa umilisi walifanya makosa ya kisarufi katika maumbo ya maneno ya Kiswahili kama ifuatavyo.

4.3.1. Kutenganisha Maneno Visivyo

Wanafunzi walitenganisha maneno mara mbili kimakosa. Kutokana na data yetu, maneno ambayo yalitenganishwa ni vitenzi ambavyo vimeongezewa viambishi mwanzoni kabla ya mzizi kama vile tunapo—fanya. Tazama Jed. 12, linadhihirisha namna wanafunzi walitenganisha maneno marefu ili yawe mawili wasipojua walisababisha makosa ya kisarufi na kuvuruga maana ya maneno hayo. Matokeo haya yanashadidia maoni ya Kemunto (2017), anaposema kuwa wanafunzi wengi hutatizika na maneno yaliyo marefu sana kiasi cha kufikiria kuyatenganisha ili yawe mawili au zaidi. Mbaabu (1995) anasema kuwa umbo la neno ambalo hutenganishwa huwa na mzizi wa vitenzi.

Jed. 12. Maneno Yaliyotenganishwa Visivyo

Neno sahihi	Neno lenye athari
Anajipenda	Ana—jipenda
Tunapofanya	Tunapo—fanya
Hupenda	Hu—penda
Hunifunza	Huni—funza
Kuwakataza	Kuwa—kataza

4.3.2. Kuunganisha Maneno Visivyo

Wanafunzi walifanya makosa ya kuunganisha maneno mawili na kuyafanya kuwa kama neno moja. Maneno ambayo yaliunganishwa ni kihusishi + nomino kama vile [wa/darasa] na nomino + kivumishi [kaka/wawili] kama inavyodhihirika katika Jed. 13. Katika Jed. 13 vilevile mofimu ambazo hujisimamia kimaana zimeunganishwa kama vile: nomino (darasa), kihusishi (wa) na kivumishi (wawili).

Jed. 13. Maneno yaliyounganishwa Visivyo

Neno sahihi	Neno lenye athari
Wa darasa	Wadarasa
Wa kiume	Wakiume
Wa kike	Wakike
Kaka wawili	Kakawawili
Kwake vitabu	Kwakevitabu

Uunganishaji huu ulisababisha makosa katika maneno ya Kiswahili kutokana na hali kuwa wanafunzi walishindwa kutambua maneno yapi yanastahili kuunganishwa na yapi hayastahili kuunganishwa. Katika utafiti huu, ni dhahiri kuwa uunganishaji ulihusu nomino na vivumishi na kihusishi na nomino. Uunganishaji huu hata hivyo ni wa kimakosa. Kemunto (2017) anashadidia kuwa baadhi mofu za Kiswahili huweza kujisimamia ilhali nyingine haziwezi. Anaeleza kuwa wanafunzi waliunganisha mofu ambazo hujisimamia zenyewe kama vile nomino + kivumishi, nomino + kiunganishi, nomino + kihusishi na kitenzi + kielezi.

Jed. 14. Kudondosha Silabi katika Neno

Neno sahihi	Neno lenye athari
Wanyama	Wanya^
Uhusiano	U^siano
Wali	Wa^
Mmoja	M^ja
Ninaenda	^nenda

4.3.3. Kudondosha Silabi katika Neno.

Wanafunzi walidondosha silabi mwishoni mwa neno kama vile [Wanya[^]] katikati mwa neno [u[^]siano] na mwanzoni mwa neno [nenda[^]]. Jed. 14 linaonyesha hali hii.

Matokeo haya yanalingana na maoni ya Kemunto (2017) anayesema kuwa wanafunzi huacha silabi katika maandishi ya maneno fulani kutokana na upungufu wa umilisi wa viambishi katika Kiswahili. Kwa mujibu wa utafiti huu, ukosefu wa makini na kuandika kwa haraka kwa mwanafunzi vilevile huchangia kuacha silabi katika neno na husababisha makosa katika neno husika. Hali hii ilishuhudiwa katika insha za wanafunzi wa mtaala wa umilisi katika uandishi wa insha zao. Makosa ya udondoshaji yameainishwa na kuchanganuliwa kama anavyopendekeza Al-khreshah (2016).

4.4. Makosa ya Sarufi Miundo.

Omar (2022), anaeleza kuwa sarufi miundo ni utanzu wa sarufi unaojishughulisha na uchanganuzi wa mpangilio wa maneno katika sentensi na uhusiano wa vipashio vyake. Makosa ya sarufi miundo yalidhihirika katika upatanisho wa kisarufi.

4.4.1. Makosa ya Upatanisho wa Kisarufi.

Utafiti ulibaini kuwa wanafunzi walishindwa kupatanisha viambishi vinavyofaa katika maneno na sentensi na hivyo kusababisha makosa ya upatanisho. Makosa hayo yamenakiliwa katika Jed. 15 ambalo linaonesha sentensi zenye makosa kutokana na wanafunzi wa mtaala wa umilisi kushindwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi.

Jed. 15: Makosa ya Upatanisho wa Kisarufi

Sentensi sahihi	Sentensi yenye athari
Anaupenda mwili wake	Anaipenda mwili yake
Ana meno meupe	Ana meno nyeupe
Ana baba mmoja na mama mmoja	Ana baba moja na mama moja
Eneo la Butula	Eneo ya Butula

Kutokana na Jed. 15, wanafunzi walishindwa kupatanisha maneno katika sentensi kutegemea ngeli husika. Wanafunzi waliandika (meno nyeupe) badala ya (meno meupe) hii inaonesha kuwa mwanafunzi huyo hatambui kuwa katika maneno ya ngeli ya LI-YA, kiambishi (me-) hupatanishwa kama kiambishi tangulizi katika sentensi hali ya wingi. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Obara (2014) anayesema kuwa katika Kiswahili sanifu, ngeli ya nomino huathiri upatanisho wa viwakilishi, vivumishi na vitenzi katika sentensi.

Makala hii yalibaini kuwa wanafunzi wa shule za msingi wa mtaala wa elimu ya umilisi wanaojifunza Kiswahili hufanya makosa ya upatanisho wa kisarufi kutokana na upungufu wao wa umilisi wa viambishi na matumizi ya ngeli. Kwa hiyo walimu wao wanastahili kutilia maanani ufunzaji wa viambishi na ngeli na matumizi yake.

Haroon (1998), aligundua kuwa Kigisu kiliathiri mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiswahili. Anasema kuwa, kutokana na tofauti za kimuundo kati ya lugha hizi mbili, watafitiwa walihamisha muundo wa nje

wa kisintaksia wa lugha yao kwa lugha ya pili (Kiswahili). Hali hii ilikuwa chanzo cha makosa aliyogundua Haroon (1998) katika mpangilio wa maneno katika sentensi zilizotungwa na watafitiwa husika.

4.5. Makosa ya Sarufi Maana

Mekacha (2011) anaeleza kuwa sarufi maana (semantiki) ni taaluma inayochanganua na kufafanua miundo na mifumo ya maana na kipashio chake cha msingi katika uchanganuzi wa leksimu na umbo lenye maana moja. Makosa ya kisemantiki yalidhihirika katika insha za wanafunzi wa mtaala wa umilisi. Wanafunzi walifanya makosa haya ambapo sentensi ilikosa kutoa maana iliyokusudiwa. Makosa ambayo wanafunzi walifanya ni kama yafuatayo:

4.5.1. Matumizi ya Msamiati Usiofaa

Utafiti ulibaini kuwa maneno yanayokaribiana kimaana yalitumiwa katika sentensi kwa njia isiyofaa katika muktadha husika na kuzua dosari za kimaana

Jed. 16: Matumizi ya Msamiati Usiofaa

Sentensi sahihi	Sentensi yenye athari
Yeye hufanya vyema katika mtihani	Yeye hunga vyema katika mtihani
Yeye ni mweupe pepepe	Yeye ni mweupe tititi
Yeye si mnene wala mkonde	Yeye si mnono wala mkonde
Tuliabiri gari	Tulipanda gari

Katika Jed. 16 kuna matumizi yasiyofaa ya istilahi zinazozua dhana potofu. Neno tulipanda kwa mfano limetumika badala ya tuliabiri. Hali hii inazua dosari za kimaana na hivyo kusababisha makosa ya kisemantiki. Makosa ambayo wanafunzi wa Kimarachi walifanya yalitokana na ujuzi wa lugha ya kwanza ya wanafunzi kwa mfano neno hunga si la Kiswahili.

Mifano mingine “mnono na mweupe tititi” inazua dosari za kisemantiki. Katika Nadharia ya Sarufi Zalishi, Chomsky (1957), anadai kuwa mwanafunzi atatumia ujuzi alionao katika lugha asilia kujieleza katika lugha lengwa. Hali hii ni sawia na makala haya ambapo wanafunzi walitumia ujuzi wa lugha ya Kiamarachi katika kujieleza katika lugha ya Kiswahili. Jambo hili lilizua makosa ya kisemantiki katika insha za wanafunzi.

4.5.2. Kuongezwa kwa Maneno katika Sentensi

Kosa lingine lilitokana na watafitiwa kuongeza maneno yasiokuwa na maana katika sentensi na kuvuruga maana ya sentensi hiyo. Maneno haya yanastahili kuondolewa katika sentensi ndiposa sentensi hiyo itoe maana iliyokusudiwa. Jed. 17 linaonesha kuongezwa kwa maneno yasiyokuwa na maana katika sentensi kulingana na muktadha.

Jed. 17: Maneno yaliyoongezwa kimakosa

Sentensi sahihi	Sentensi yenye athari
Yeye si mrefu wala mfupi	Yeye si mrefu wala si mfupi
Walemavu na maskini	Walemavu na wenye ni maskini
Hupenda kucheza	Hupenda kucheza mchezo wa
kandanda na kusoma	kandanda pia yeye hupenda
hadithi	kusoma hadithi
Watoto na watu ambao	Watoto pia na watu ambao
wanamshinda umri	wanamshinda umri

Jed. 17 linaonesha maneno yaliyoongezwa kimakosa katika sentensi, kama vile sentensi (*Yeye si mrefu wala

si mfupi) neno si limeongezwa kimakosa katika sentensi, neno hilo linastahili kuondolewa katika sentensi ndiposa sentensi hiyo iwe na maana.

Matokeo haya yanalingana na mawazo ya [Kemunto \(2017\)](#) anayesema kuwa mwanafunzi hutumia kiambajengo kimakosa katika sentensi. Makosa haya hutokea wakati mwanafunzi hajui mahali mwafaka pa kutumia kiambajengo husika katika sentensi. Udhafu huu hutokea mwanafunzi anaposhindwa kubainisha nafasi na matumizi mwafaka ya viambajengo vya sentensi huhusishwa na lugha ya pili (Kiswahili)

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Makosa katika kutambua na kuainisha makosa ya kisemantiki katika sentensi za wanafunzi wajifunzaji wa Kiswahili wazungumzaji wa kimarachi wa mtaala wa umilisi. Nadharia hii inadai kuwa makosa katika wajifunzaji wa lugha hutatiza mawasiliano. Kutokana na makala hii, ni dhahiri kuwa wanafunzi walitekeleza makosa anuai ya kisarufi. Makosa haya yalidhihirika katika viwango vyote vya kisemantiki

5. Hitimisho

Makala hii inahitimisha kuwa makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa Kiswahili katika mtaala wa elimu ya umilisi ambao lugha yao ya kwanza ni Kimarachi ni mengi na yanajumuisha makosa ya sarufi sauti, sarufi maumbo, sarufi miundo na sarufi maana. Ingawa makosa mengi yalitokana na athari ya lugha ya kwanza mengine yametokana na vyanzo mbalimbali. Iwapo mikakati mwafaka itatumika kukabili tatizo hili, wanafunzi wataweza kuepuka makosa mengi. Ufunzaji kwa mtindo wa elimu ya umilisi ni mkakati mwafaka wa kurekebisha makosa haya.

Ili kupunguza au kutatua tazizo la makosa ya Kisarufi, Makala hii inapendekezo yafuatayo:

- i. Ni muhimu mwalimu kuwa na njia mwafaka ya kukosoa insha za wanafunzi. Mathalani, kosa la kudondoa herufi lioneshwe kutumia alama achwa (^), kosa la kuongeza herufi lioneshwe kwa alama nyongeza (+) ama lipigiwe vijistari viwili chini yake na lile la kubadilishana sauti lipigiwe kijistari kimoja. Kisha mwalimu anafaa kuwaelekeza wanafunzi kujua aina ya makosa na alama zinazotiwa kwa kila kosa. Pia anafaa kutoa marejeleo ya vitabu vinavyoshughulikia vipengele vinavyowatatiza wanafunzi.
- ii. Matumizi ya mbinu na vifaa bora vya ufunzaji na ujifunzaji wa insha na walimu yanahimizwa. Mbinu ya ukosoaji wa moja kwa moja inapendekezwa kutumiwa na mwalimu. Mbinu hii ni mwafaka kwa pande zote kwa sababu humsaidia mwanafunzi kugundua makosa yake papo hapo na kuyarekebisha. Walimu Pamoja na wanafunzi wanahimizwa kutumia mtandao katika kufanya utafiti zaidi kuhusu uandishi wa insha. Mbinu hii itawasaidia walimu na wanafunzi kuwa na mawanda mapana kuhusu uandishi wa insha jinsi inavyopendekezwa na wizara ya elimu katika elimu ya umilisi.

- iii. Walimu wanahimizwa kuwaelekeza wanafunzi kutambua miundo ya lugha ya Kiswahili na lugha asili ya wanafunzi. Kila lugha ina miundo yake tofauti, kwa hivyo itakuwa vyema ikiwa tofauti za kimuundo baina ya lugha ya Kiswahili na lugha ya kwanza zitafundishwa kusaidia wanafunzi kuepuka baadhi ya makosa.
- iv. Wizara ya elimu iweze kufuatilia na kuchunguza namna walimu wanavyofunza shuleni kwa kuzingitia stakabadhi, nyenzo na vifaa vinavyohitajika kufanikisha somo.

MAREJELEO

- Akoth, B. K. (2014) Uchanganuzi Makosa na Muundo Sentensi: Ulinganisho wa Sentensi Sahili za Kiswahili Sanifu na za Kisuba. Tasnifu ya Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Al-khresheh, M. H. (2016). A Review Study of Contrastive Analysis Theory, In International Journal of Humanities and Social Sciences.
- Bakita (2015). Kamusi Kuu ya Kiswahili. Dar es Salam, Longhorn.
- Chomsky, N. (1957). Syntactic Structures. The Hague: Mouton.
- Corder, S. P. (1967). The Significance of Learner's Error. International Review of Applied Linguistics
- Cross, S. (2009) Diagnosing the Process, Text and Intrusion Problems Responsible for L2 Listeners' Decoding Errors. In the Asian EFL Journal Quarterly. Vol. 2 Issue (UK. 47-50) Asian EFL Journal Press, Busan, Korea.
- Guthrie, M. (1971). Comparative Bantu: An Introduction to the Comparative Linguistics Pre-history of the Bantu Language. Vol 2. Farnborough: Gregg Press.
- Haroon, M. (1998). Kuathirika kwa Kiswahili na Kigisu Nchini Uganda Kifonolojia, Kimofolojia, Sintaksia na Utamaduni. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa). Kampala University Press.
- Kemunto, B.A. (2017). Makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili: mfano wa kaunti ya kakamega.
- Kiango, J.G. (2002). Nafasi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Jamii Mpya ya Afrika Mashariki. Dar es Salam: Baraza la Kiswahili la Taifa.s
- Kisakwah, B. A. (2014). Uchanganuzi makosa na muundo sentensi: ulinganisho wa sentensi sahili za kiswahili sanifu na za kisuba.
- Kombo & Tromp. (2006). Proposal and Thesis Writing. Nairobi: Paulines Publications Africa.
- Massamba, D. P. B. (2016). Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha. Dar es Salaam: TUKI.
- Marshall, M. (1996). Sampling for Qualitative Research; Family Practice, 13(6) 522-525.
- Mashaka, W. (2015). Athari za lugha ya Kijita katika

kujifunza Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili ambayo haijachapishwa. Chuo kikuu cha Huria Tanzania.

Mbaabu, I. (1995) Usahihishaji wa Makosa katika Kiswahili. Nairobi: Longhorn Kenya Ltd.

Mekacha, R.D.K. (2011). Isimu jamii: Nadharia na muktadha wa Kiswahili Minocity: Osaka University of Foreign Studies.

Mushumbwa, A.R. (2020). Makosa Ya Kisarufi Katika Makala Andishi Za Habari: Uchunguzi Kifani Wa BBC Swahili Na DW Kiswahili.

Nyagah, K.S. (2016). Uchanganuzi wa makosa ya Kifonolojia na Kimofolojia yaliyojitokeza katika kazi andishi za wanafunzi wa shule za upili, Tigania, Jimbo la Meru; Chuo kikuu cha Nairobi.

Obara, M.J. (2014). Uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya ekegusii. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Omar, N.A. (2022). Uchanganuzi wa Makosa ya Kimofolojia ya Wanafunzi wa Kiwaata Wanapojifunza Lugha ya Kiswahili. Pwani University, 2022.

Otiende, M. A. (2013). Athari za Mofonolojia ya Kibasuba katika Matumizi ya Kiswahili kama Lugha ya Pili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sridhar, S. N. (1981). Constrastive Linguistic and Language teacher. Oxford: Pergamon. Retrieved May 30, 2014 from <http://www.unb.br/let/graham/conon/htm>

Wairimu, V. G. (2016). Athari za Kifonolojia za Lahaja ya Kiamu na Kitikuu katika Kiswahili sanifu; Chuo Kikuu cha Nairobi.

Wenceslaus, M. (2015). Athari za Lugha ya Kijita katika Kujifunza Kiswahili. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.